JINA LA MWANAFUNZI _____

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI ENG. STELLA MANYANYA
MTIHANI WA MUHULA WA PILI KIDATO CHA KWANZA

021 **KISWAHILI**

MUDA:SAA 02:30 **NOVEMBA 2026**

MAELEKEZO

1. Karatasi ina sehemu A, B na C yenye jumla ya maswali 10

2.Jibu maswali yote

3. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi

4. Vifaa vyote vya mawasiliano visiruhusiwe katika chumba cha mtihani

5.Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi ulizopewa

6.Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia

JINA LA MWANAFUNZI _____

SEHEMU A (Alama 15)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Katika kipengele (i) - (x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku ulichopewa.

(i) Aina gani ya neno hutoa taarifa kuhusu tendo linalotendeka?

A Kielezi B. Kihusishi

C Kitenzi D. Kivumishi

(ii) Zifuatazo ni hoja sahihi kuhusu umuhimu wa kujifunza somo la Kiswahili **isipokuwa**:

A Kuwasiliana kwa lugha fasaha ya Kiswahili

B Kuwasiliana kulingana na rniktadha mbalimbali

C Kukuza ubunifu katika nyanja ya sarufi na fasihi

D Kukuza uvumbuzi wa teknolojia mpya za kisasa

(iii) "Shina la mti limekaa vibaya". Neno lililopigiwa mstari ni kielezi cha aina gani?

A Namna B Mahali

C Wakati D Idadi

(iv) Kurasa za rnwisho katika kamusi ambazo huorodhesha maneno na maana zake huitwaje?

A Utangulizi B Sherehe

C Kitomeo D Kidahizo

(v) Mpangilio sahihi wa muundo wa insha ni upi?

A Kichwa, mwanzo, wazo na kiini

B Kiehwa, wazo, hitimisho na kiini

C Kichwa, mwanzo, kiini na hitimisho

D Kiehwa. mwanzo, wazo na hitimisho

(vi) Neno lipi kali ya haya yafuatayo lina mofu-ya mtendwa?

A Aliyetembelea B Alimtembelea

C Atakayetembea D Ametembea

(vii) Katika uandishi wa barua ya kirafiki, anwani ya mwandikiwa huandikwa sehernu gani?

A Kona ya juu kulia ya barua B Ndani ya bahasha ya barua C Kona ya juu kushoto ya barua D Juu ya bahasha ya barua

(viii) Kusoma kwa sauti kuna faida gani kati ya zifuatazo?

A Huhainisha uwemo wa kutamka maneno kwa lafudhi sahihi

B Huonesha uwezo wa kusoma majarida na magazeti

C Hubainisha uwezo wa kusoma maandishi ya kifasihi

JINA LA MWANAFUNZI _____

D Hubainisha uwezo wa kusimulia hadithi fupi na ndefu

ix) Maana na dhana zinazobebwa na maneno ya lugha yoyote hutokana na nini?

A Idadi ya misamiati iliyopo katika lugha
B Uwezo wa watumiaji wa lugha husika
C Utamaduni na mazingira ya jamii
D Mpangilio wa sauti za lugha husika

(x) Kwa nini mawasiliano ya ana kwa ana ni halisi zaidi?

A Huhusisha matumizi ya simu
B Huhusisha ishara za mwili
C Huhusisha matumizi ya mtandao
D Huhusisha matumizi ya sauti

2. Oanisha maelezo kuhusu vipengele vya uandishi wa barua ya kirafiki katika Orodha A na vipengele husika kutoka Orodha B, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku ulichopewa.

Orodha A	Orodha B
(i) Humsaidia mwandikiwa kujua barua iliandikwa (ii) Huonesha maskani ya mwandishi. (iii) Salamu za awali zinazozingatia uhusiano uliopo baina ya mwandishi na mwandikiwa. (iv) Salamu za kuagana. (v) Madhumuni au tengo la barua husika.	A Anwani ya mwandikiwa B Anwani ya mwandishi C Kichwa cha barua D Kiini cha barua E Mwanzo wa barua F Mwisho wa barua G Tarehe ya barua

Majibu

Orodha A	(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)
Orodha B					

SEHEMU B (Alama 70)

Jihu maswali yote katika sehemu hii.

3. Soma kifungu cha habari kifuataeho kisha jibu maswali yanayofuata:

Elimu ni msingi muhimu katika maendeleo ya jamii yoyote ile. Jamii inayothamini eiimu huwa na watu wenye maarif2 na ujuzi unaowawezegha kukabiliana na changamoto

mbalimbali za maisha. Katika nchi yetu, juhudi kubwa zimefanyika kuhakikisha watoto wote wanapata haki ya elimu ili kujenga taifa lenye maendeleo endelevu.

Serikali pamoja na wazazi wana wajibu wa kushirikiana katika kuhakikisha watoto wanapata eiimu bora. Wazazi wanapaswa kuwahimiza watoto wao waende Shule na kujifunza kwa bidii. Walimu nao wanapaswa kufundisha kwa ufanisi na kuwaongoza wanafunzi katika maadili mema. Ushirikiano huu huleta matokeo mazuri katika elimu ya wanafunzi.

Juhudi za pamoja kati ya serikali, wazazi na jamii zinafanywa kwa lengo la kuendeleza elimu nchini. Serikali huhakikisha vifaa vya kujifunzia vinapatikana kwa utoshelevu na mazingira ya Shule kuwa ni raflki kwa kujifunzia. Kwa upande mwingine, wazazi huwapatia watoto mahitaji muhimu ili kuwapa motisha ya kusoma. Hali hii inaongeza tija na kupanua elimu nchini kwa kiasi kikubwa.

Hata hivyo, ni muhimu kwa kila mwanajamii kutambua kuwa elimu si kwa ajili ya mtu binafsi tu bali ni kwa faida ya taifa zima. Mtu aliyeelimika anaweza kuchangia katika maendeleo ya uchumi, afya na teknolojia. Hivyo, tunapaswa kuipa elimu kipaumbele ili kujenga taifa lenye ustawi na mafanikio ya kudumu.

Maswali

(a) Andika kichwa cha kifungu cha habari ulichosoma kwa maneno yasiyozidi matano.

_____

_____

(b) Elezea maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari ulichokisoma:

(i) Msipgi

_____

_____

(ii) Changamoto

_____

_____

(iii) Motisha

_____

(iv) Kipaumbele

(c) Nani wana jukumu la kuhakikisha watoto wanapata elimu bora kwa mujibu wa habari uliyosoma? Bainisha wahusika wawili.

(i) _____

(ii) _____

(d) Bainisha mchango wa serikaii unao;enga kukuza maendeleo ya climu nchini kulingana na habari uliyosoma kwa kutoa hoja mbili.

(i) _____

(ii) _____

(e) Kutokana na habari uliyosoma, mtu aliyeelimika hutambulikaje?

_____

_____

_____

4. "Maana ya sentcnsi za Kiswahili hukamilishwa na matumizi ya kiimbo katika maneno." Bainisha kiimbo kilichotumika katika kipengele (i) — (x), kwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika kisanduku kisha uliandike katika nafasi ya majibu uliyopewa. Jibu linaweza kutumika zaidi ya mara moja.

Maelezo, amri, Mshangao, Swali

JINA LA MWANAFUNZI _____

(i) Lo! Bara la Afrika limejikomboa! _____

(ii) Bwana Mkubwa, toka hapo utaumia. _____

(iii) Hivi tutaweza kuvuka mto huu uliofurika? _____

(iv) Ama kweli amani haiji ila kwa ncha ya upanga! _____

(v) I eta boti ufukweni tupande. _____

(vi) Usipoziba ufa, utajenga ukuta _____

(vii) Mto huu ni mkubwa Sana. _____

(viii) Baraka, ponda mali acha ubahili _____

(ix) Hapo kuna uhakika wa mavuno? _____

(x) Heri nusu Shari kuliko shari kamili. _____

5. Kwa kutumia hoja tano fafanua umuhimu wa kutumia lugha fasaha katika mawasiliano.

(i)

_____

(ii)

_____

_____

(iii)

_____

_____

(iv)

_____

_____

(v)

_____

JINA LA MWANAFUNZI _____

_____

6. Badili sentensi (i) — (vi) kwa kuzingatia maelekezo yaiiyowekwa kwenye mabano. Sentensi (i) imetumika kama mfapo.

(i) Vitabu vyetu vimesafirishwa kwa magari. (umoja) Jibu: <u>Kitabu chetu kimesafirishwa kwa gari.</u>

(ii) Kalamu ya wino mweusi inaandika vizuri. (wingi)

_____

(iii) Darasa letu lina ubao mweusi wa kuandikia. (wingi)

_____

(iy) Viongozi wa ofisi ya mazingira wamefika. (umoja)

_____

_____

(v) Shule inafanya usaili kupata mwaiimu wa Kiswahili. (wingi)

_____

(vi) Leo tutaosha magari na nyumba zetu. (umoja)

_____

7. Andika upya sentensi (ii) - (vi) kwa kutumia viunganishi vilivyopo katika kisanduku.Sentensi (i) imetumika kama mfano.

ingawa, lakini, tena, wala, bali, kama, hadi. na

(i) Mama anapika maandazi. Mama anapika mikate. Jibu.• <u>Mama anapika maandazi na mikate.</u>

(ii) Kabura fika hapa kesho asubuhi mapema. Kabura uje na mdogo wako mapcma.

_____

(iii) Mimi nitaingia darasani leo. Mimi nina homa leo.

JINA LA MWANAFUNZI _____

_____

(iv) Fatuma hamwogopi mwalimu wake. Fatuma anamuheshimu mwalimu wake.

_____

(v) Mama atapona vizuri. Marna atameza dawa alizopewa.

_____

(vi) Rashidi anaishi mbali. Rashidi namuonea huruma.

_____

8. Bainisha vishazi tegemezi katika sentensi zifuatazo kwa kuviandika katika nafasi iliyoachwa wazi kwa kila kipengele.

(i) Wanafunzi watafaulu wakisoma kwa bidii.

_____

(ii) Sisi hatukuvutiwa alivyosoma.

_____

(iii) Aliponiona alipiga kelele.

_____

(iv) Jalada lililofunguiiwa limefungwa.

_____

(v) Mahati alimolala mgeni mna kunguni wengî.

_____

9. Ukiwa kama Katibu wa serikali ya wanafunzi katika shule yako, unalo jukumu la kuandika kumbukumbu za vikao vya shule. Kwa kutumia mifano, fafanua vipengele vitano utakavyovizingatia katika uandishi huo.

(i) _____

_____

(ii) _____

_____

(iii) _____

_____

(iv) _____

_____

(v) _____

SEHEMU C (Alama 15)
Jibu swali la kumi (10).

IO. Umebaini kuwa wanafunzi wenzako hutumia muda mwingi katika mitandao ya kijamii kuangalia mambo yasiyofaa. Andika insha yenye maneno yasiyopungua 200 na yasiyozidi 250 yenye kuwaelimisha wanafunzi hao kuhusu madhara ya mitandao hiyo.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

JINA LA MWANAFUNZI _____